**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

MARA REGION:
Telephone No:. 028 2620984
**Email Address: acl.mara@lands.go.tz.**

Ofisi ya Ardhi Mkoa,
Mkoa wa Mara,
S.L.P. 495,
**Musoma.**

**Kumb, Na. LD/MR/GF/8 VOL.1/01** **12/12/2022**

BARAZA LA UHIFADHI WA MAZINGIRA (NEMC),
KANDA YA ZIWA,
S.L.P 11045,
MWANZA

**YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA ZBS INVESTMENT LTD AMBAYO INAMPANGO WA KUANZA UJENZI WA PANELI YA JUA (SOLAR PLANT) ENEO LA NYASORO WILAYA YA RORYA**

Husika na mada tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Mara imepokea barua kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rorya kuhusiana na ombi la kuitambulisha Kampuni tajwa hapo juu,katika Ofisi yako ili iweze kupata cheti cha Mazingira kutoka Ofisi yako.

3. Aidha, kwa barua hii tunaitambulisha kwako Kampuni hii, ikiwa ni lengo la kuendelea na taratibu zingine zinazofuata. Pamoja nabarua hii naambatanisha kwako muhtasali wakikao cha Halmashauli ya Kijiji na barua toka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kwa ajili ya rejea.

Nakutakia utekelezaji mwema.

Kitumbika, AM
**Kny: Kamishna wa Ardhi Msaidizi**

**Nakala:** ZBS INVESTMENT LTD
S.L.P 1242
**Dar es Salaam.**

Scanned with CamScanner

Certified as True Copy of the Original
Fikiri Liganga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 17/11/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**

Jnapojibu tafadhali taja

**Kumb. Na. HWR/DLO/RA/55/VOL.B/24** **Tarehe: 08/12/2022**

KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI
MKOA WA MARA
S.L.P 495
**MUSOMA**

**YAH: MATUMIZI YA ENEO KWAAJILI YA UJENZI WA PANEL YA JUA (SOLAR PLANT)ENEO LA NYASORO WILAYA YA RORYA**

afadhali rejea somo la hapo juu.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wilaya ya Rorya inakiri kupokea ombi la Kampuni ya **ZBS vestments Ltd wa S.L.P 1242 Dar es salaam** kutaka kupewa kibali cha paneli ya jua neo la Nyasoro wilaya ya Rorya.

Baada ya kupokea, maombi hayo tulifanya ukaguzi na kubaini mambo yafuatayo;

i. Eneo husika halijapimwa wala kuwekewa alama za kudumu.
ii. Eneo husika linamilikiwa kiasili na Kampuni ya **ZBS Investments Ltd** walilolipata kwa kununua kutoka kwa wakazi wa asili.
iii. Matumizi ya ardhi yaliyopendekezwa na serikali ya kijiji na wananchi kwa ujumla yatasaidia kuongeza nishati ya mwanga kwa wananchi wanaozunguka na wilaya jirani ya Tarime hasa ukizingatia eneo tajwa halijafikiwa na nishati ya umeme.
iv. Aidha, tumepokea maombi ya upimaji wa eneo toka kwa wamiliki wa Kampuni na tayari taratibu za upimaji zinaendelea.
v. Eneo hili, linaukubwa wa ekari 34 kwenye jira(Cordinates) zifuatazo;
   - 637340.46, 9848115.98
   - 637138.80,9848136
   - 637106.9, 9848117
   - 636967.7, 9848102
   - 636952.3, 9848072
   - 637011.8, 9847707
   - 637365,9847719
   - 637350, 9847871
   - 637302.6, 9847870
vi. Kiwanja hiki hakina mgogoro wowote wa mipaka au mgogoro mwingine na majirani zake.

Certified as True Copy of the Original
Fikiri Liganga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: ..............
Date: ..............



Scanned with CamScanner

vii. Kampuni imeingia makubaliano na serikali ya kijiji katika kuchangia kuimar kuboresha huduma za jamii kama shule, maji nk

4. Baada ya kujiridhisha juu ya masuala yote tajwa hapo juu, tunashauri Kampuni Investments Ltd ipewe usaidizi wa kutambulishwa na **Mamlaka ya Uhifadhi wa Mazi kuweza kupata cheti cha mazingira kwa ujenzi.**

Naomba kuwasilisha.

TP.Fredy Kyalawa
***Kny MKURUGENZI MTENDAJI (W)***
***RORYA.***

**Nakala:**

i. Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
S.L.P 250
**Rorya/ Tarime** - Aione kwenye jalada.

ii. ZBS Investments Ltd
S.L.P 1242
**Dar es salaam** - Kwa taarifa

iii. Baraza la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC)
Kanda ya Ziwa
S.L.P 11045
**Mwanza**

Scanned with CamScanner

Certified as True Copy of the Original
Fikiri Liganga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: ...............
Date: 17/4/2022

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

SIMU NA: 027 – 2552000
MOB NA: 0677 - 010213
FAX NA: 027 - 2552020
Email: ded@kitetodc.go.tz
info@kitetodc.go.tz

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W).
S.L.P. 98,
KIBAYA - KITETO

**KUMB.NA. AR/K/343/VOL 1V/ 156** **15/12/2022**

MENEJA WA KANDA,
BARAZA LA USIMAMIZI WA MAZINGIRA TAIFA,
S.L.P 2724 PSPF PLAZA,
DODOMA.

**YAH: MATUMIMZI YA ENEO KWA AJILI YA UJENZI WA PANELI YA JUA (SOLAR PLANT) LILILOKO KATIKA KIJIJI CHA MDUNKU KATA YA ENGUSERO.**

Kampuni ya ZBS yenye Makao Makuu yake Dar es salaam inatarajia kuwekeza katika Wilaya ya Kiteto katika Kijiji cha **Mdunku Kata ya Engusero**.Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji iliwapokea wataalam kutoka kampuni ya ZBS inayojihusisha na masuala ya ufuaji wa umeme jua. Katika kutekeleza mradi huo watalaamu hao walieleza kuwa kuna eneo ambalo katika utafiti wao wameona linafaa kujenga mitambo hiyo ya kuzalisha umeme wa jua.

Kwa sababu hiyo waliomba mtalaamu Kutoka Ofisi ya ardhi na Mtaalamu kutoka Ofisi ya Mazingira kuambatana Pamoja nao Kwenda kuliangalia eneo hilo kama linafaa. Ombi lao lilikubaliwa na tulikubaliana wakati tunaenda kuliona eneo ni muhimu uongozi wa serikali ya Kijiji ukapewa taarifa, jambo ambalo lilifanyika kama tulivyo kubaliana.

Baada ya kukutana na uongozi wa Serikali ya Kijiji cha **Mdunku** walionekana kuujua mradi na waliufurahia sana. Baada ya mazungumzo ya muda mfupi, Viongozi wa kijiji walitupeleka kuona eneo ambalo limependekezwa kujenga mitambo hiyo.

Ifahamike kuwa hadi tunatembelea eneo ambalo linapendekezwa kujengwa mtambo, eneo hili lilikuwa bado ni la mwananchi (**HABIBU MBWANA MSONDE)** ambaye hadi wakati huo alikuwa bado hajalipwa chochote ili kuachia eneo, kwa hiyo eneo lilikuwa bado linamilikwa na mwananchi huyo wakati taratibu nyingine zikiendelea.

Tarehe 02/12/2022 **ZBS** na **HABIBU MBWANA MSONDE** waliingia Mkataba wa kuuziana eneo hilo ambalo lina ukubwa wa Ekari 27 kwa Fedha za Kitanzania Shilingi Milioni Ishirini na Saba **(Tsh 27,000,000/=** ambapo **ZBS** wamemlipa **Bwana HABIBU MBWANA MSONDE** Kiasi chote cha Fedha kupitia Akaunt Namba **50101600078 NMB** yenye majina **HABIBU MBWANA MSONDE.** Aidha Pamoja na barua hii naambatisha

Certified as True Copy of the Original
Fikiri Liganga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 17/4/2023

nyaraka zote zinazohusiana na ZBS kupata eneo hilo ikiwa ni Pamoja na **Bank dipost slip** kwa wepesi wa rejea

Kwa kupitia manunuzi haya eneo hili linamilikiwa na **ZBS**, Ofisi ya Mkuruggenzi Kiteto kupitia idara ya ardhi Kiteto imejiridhisha juu ya upatikanaji wa eneo hili kwa ZBS na kwa kuwa vilevile Afisa Mazingira Wilaya aliona eneo hilo linafaa kwa matumizi hayo,Kwa sasa taratibu za upimaji zinaendelea na matumizi yapo katika mipango tarajiwa ya halmashauri hivyo tunashauri kampuni ya ZBS ipewe usaidizi na ofisi yako ili waweze kuendelea na taratibu za utekelezaji wa mradi huo ambao kama halmashauri tunaamini itakuwa ni chachu ya maendeleo ndani ya wikaya yetu.

Katika Utumishi wa Umma.

**Goodluck kyando**
**Afisa Ardhi Mteule**
**KITETO**

**NAKALA:** Kamishina msaidizi wa ardhi
S.L.P 621
Babati. Kwa taarifa

ZBS Investment LTD
S.L.P 1242
Dar es Salaam. Kwa taarifa na wepesi wa ufuatiliaji.

Certified as True Copy of the Original
Fikiri Liganga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: ...............
Date: 17/4/2023